

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA SITA

13 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA


KIKAO CHA SITA – TAREHE 13 APRILI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

49. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa na Wataalam wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Malawi ambayo ipo Kata ya Buza Temeke.

50. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga nyumba za Walimu katika Halmashauri ya Ikungi.

WIZARA YA AFYA:

51. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itafunga Mtambo wa Mashine ya Oxygen katika Hospitali ya Rufaa ya Iringa ili kuhudumia Wagonjwa wa dharura.

WIZARA YA NISHATI:

52. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa umeme wa Upepo Singida utaanza.

WIZARA YA KILIMO:

53. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuwavutia Wawekezaji katika Kilimo cha Zao la Muhogo Wilayani Muheza.

54. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini miradi ya umwagiliaji katika Vijiji vya Nyamterela na Katunguru pamoja na Vijiji vya Kwindi na Isole itakamilika Wilayani Sengerema.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

55. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-


Je, ni lini Serikali itafungua Tawi la Chuo Kikuu cha Sokoine Wilayani Tunduru kwa kuwa Majengo yake yamekamilika kwa asilimia 65.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

56. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itaunda tena Bodi ya Wataalam wa Ugavi na Ununuzi (PSPTB) baada ya kuvunjwa kwa muda mrefu.



WIZARA YA MAJI:

57. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji katika Manispaa ya Morogoro.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
13 APRILI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE